

300 Mungu awabarikie nyote na awe pamoja nanyi!

1. Mungu awabarikie nyote na awe pamoja nanyi! Awalinde kwa amani!

Pambio:

Mungu n'awe nanyi siku zote! Mungu n'awe nanyi daima hata mwisho wenu wa safari! Mungu n'awe nanyi daima hata tuonane huko juu!

2. Mungu wetu awalinde pote na kuwahifadhi vema kwa mikono ya rehema! Mungu n'awe nanyi siku zote!

3. Mungu awaangazie nuru, na awashibishe sana kwa fadhili zake Bwana! Mungu n'awe nanyi siku zote!

4. Mungu awainulie uso! Na wakati wa kuhama mpelekwe kwa salama! Mungu n'awe nanyi siku zote!

5. Mungu awabarikie nyote, awalinde m-we huru, awaangazie nuru! Awainulie uso wake!

J.E. Rankin / Daniel Hallberg

God be with you till we meet again, R.S. 942; R.H. 722